

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

HATIMAYE MTANDAO WA “MAKING FINANCE WORK FOR AFRICA” (MFW4A) WAZINDULIWA RASMI NCHINI ABIDJAN LEO

Mtandao wa www.mfw4a.org, umezinduliwa leo majira ya saa moja na nusu asubuhi na jopo la wataalamu wa mambo ya fedha Afrika.

Akizungumza katika mkutano huo uliochanganya waandishi wa habari na maafisa mbalimbali, Bw. Stefan Nalletamby alisema kuwa, madhumuni ya mkutano huu wa asubuhi ni kuzindua tovuti hii na kuwaonyesha jinsi mtandao huu unavyofanya kazi. Hii itawasaidia kujua kuwa ni vyanjo gani vya hela vinatolewa na ni kwa nani. Alizungumza Bw. Nalletamby ambaye ni mratibu wa ushirikiano wa MFW4A.

Aliendelea kueleza kuwa utawawezesha kuwajua wale wote wanaojihusisha na mambo ya fedha kuwa wanapata kiasi gani. Alikadhalika watunga sera yenye mamlaka kwenye nchi zao na watafiti wote katika bara letu.

Uzinduzi huo uliofanyika mapema leo asubuhi ukiongozwa na Bw. Nalletamby akishirikiana na jopo la wataalamu wa Afrika ambao ni Bw. Thomas Losse - Muller, mratibu wa programu, Bw. Gabriel Negatu, Mkurugenzi wa uchumi na Idara ya maboresho ya matumizi ya fedha na Bw. Mthuli Ncube, ambaye ni Mchumi Mkuu na Makamu wa Rais wa Benki ya Mandeleo Afrika.

Tovuti hii inaanza kutumika mara moja kwani itatoa nafasi hata kwa wale ambao wanafanya tafiti mbalimbali za mambo ya fedha na mabenki kupata urahisi wa kuwa na habari za kweli na uhakika.

Imetolewa na Msemaji Mkuu

Wizara ya Fedha na Uchumi

Abidjan

24.05.2010